

**MAKUBALIANO YA KUPANGISHA KIWANJA KWA MATUMIZI OFISI YA
BIASHARA**

MAKUBALIANO HAYA YAMEFANYIKA leo tarehe.....**31**..... Mwezi.....**03**.....2023

BAINA YA

MOZZA ALLY MOHAMED mkazi wa Chang'ombe, jijini, Dar es Salaam, Tanzania ambapo hapa anatambulika kama "Mpangishaji" kwa upande mmoja.

NA

SAID ABDALLAH ALLY mwenye anuani ya Ofisi S.L.P 16525, Dar es Salaam, Tanzania ambapo hapa anatambulika kama "Mpangaji" kwa upande mwingine.

KWA KUWA Mpangishaji ni mmiliki halali wa kiwanja kilichopo kwenye plot nambari 207 ndani ya block 18 eneo la Kibada Wilaya ya Kigamboni jijini Dar es Salaam.

KWA KUWA Mpangishaji kwa hiari yake mwenyewe amekubali kupangisha kiwanja kwa matumizi ya kuegesha magari kwa ndugu **SAID ABDALLAH ALLY** kwa makubaliano yao kama yanavyoonekana hapo chini.

SASA PANDE ZOTE MBILI WAMEKUBALIANA KAMA IFUATAVYO: -

1. Kwamba Mpangishaji amepangisha kiwanja na Mpangaji amekubali kupanga katika kiwanja hicho kwa matumizi tajwa hapo juu.
2. Kwamba mkataba huu wa kupanga utakuwa ni wa Miaka Mitano na utanza tarehe 31/03/2023 hadi tarehe 31/03/2028.
3. Kwamba Kodi kwa mwezi itakuwa ni kiasi cha Shilingi Milioni Moja (TSh. 1,000,000/=) tu.
4. Kwamba Mpangaji hataruhusiwa kufanya marekebisho ya eneo tajwa bila idhini ya Mpangishaji.
5. Kwamba Mpangaji hatakuwa na mamlaka ya kumpangisha mtu mwingine katika kipindi hicho cha Miaka Mitano na pia Mpangishaji hatakuwa na mamlaka ya kumbughudhi Mpangaji.
6. Kwamba Mpangaji akitaka kuongeza mkataba atamtaarifu Mpangishaji mwezi mmoja kabla ya mkataba kuisha. Mpangishaji atakuwa na hiari ya kukubali au kukataa kuongeza mkataba huo.

MAKUBALINO HAYA Yametiwa saina leo tarehe... 31 ... Mwezi... 03 ... 2023 mbele
ya mashaidi kama ifuatavyo:-

UMETIWA SAINI na **MOZZA ALLY MOHAMED**

ambaye amefahamishwa Mimi binafsi

na

leo tarehe 31 mwezi 03 2023

} MAMohamed
.....
MPANGISHAJI

UMETIWA SAINI na **SAID ABDALLAH ALLY**

Ninayemfahamu/ ambaye amefahamishwa kwangu na

..... Ninayemfahamu leo

tarehe 31 mwezi 03 2023.

}
.....
MPANGAJI

MBELE YANGU:

JINA: NENILE JOSEPHINE DAVID

SAINI: *Funck*

ANUANI: 3238 DAR ES SALAAM

WADHIFA: WAKILI.

